TANGAZO LA SERIKALI NA. 759 la tarehe 30/8/2024

SHERIA YA ELIMU,
(SURA YA 353)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 39)*

AMRI YA UANZISHWAJI WA BODI ZA SHULE ZA SEKONDARI ZISIZO ZA SERIKALI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uanzishwaji wa Bodi za Shule za Sekondari Zisizo za Serikali ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Amri hii itatumika kwenye Shule za Sekondari zisizo za Serikali zilizosajiliwa chini ya Sheria.

Tafsiri

3. Katika Amri hii, isipokuwa muktadha ukihitaji vinginevyo-

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Shule iliyoanzishwa chini ya aya ya 11 ya Amri hii;

"Kamishna" maana yake ni Kamishna wa Elimu au mtu mwingine yeyote ambaye amekasimishwa mamlaka ya kutekeleza majukumu ya Kamishna;

"Mkurugenzi" kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya; kuhusiana na Mamlaka ya Mji, Mkurugenzi wa Mji; kuhusiana na Halmashauri ya Manispaa, Mkurugenzi wa Manispaa na kuhusiana na Halmashauri ya Jiji, Mkurugenzi wa Jiji; na

Sura ya 353

"Sheria" maana yake Sheria ya Elimu.

Muundo wa Bodi za Shule

4.-(1) Bodi ya Shule ya Sekondari isiyo ya Serikali itajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) mmiliki wa shule au mwakilishi wake;
(b) mwalimu wa taaluma shuleni;

(c) mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wafanyakazi wanataaluma wa shule aliyeteuliwa na wafanyakazi wanataaluma wa shule na endapo shule ina kitengo kinachohusiana na wanafunzi wenye mahitaji maalumu, mkuu wa kitengo atakuwa mjumbe;

(d) wajumbe wawili walioteuliwa na wazazi wenyewe kutoka miongoni mwa wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo kupitia mkutano wa wazazi ulioratibiwa na shule ambapo mmoja kati ya wazazi hao lazima awe ni mzazi wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kama yupo;

(e) mjumbe mmoja anayewakilisha wanajamii wa eneo ambalo shule ipo na ambaye atateuliwa na mkuu wa shule; na

(f) Afisa Elimu Wilaya anayehusika na elimu ya sekondari ambapo shule ipo au mwakilishi wake.

(2) Mkuu wa shule atakuwa katibu wa Bodi.

(3) Uteuzi wa wajumbe chini ya aya hii utazingatia usawa wa jinsia.

(4) Bodi inaweza kumwalika mtu kushiriki katika kikao cha Bodi, kutegemeana na hoja ambayo itakuwa inajadiliwa na ambayo inahitaji uwepo wa mtu mwenye ufahamu na ujuzi maalumu ili kuisaidia Bodi kufanya maamuzi sahihi ila mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Muda wa ujumbe

5. Kila mjumbe wa Bodi atakuwa katika nafasi ya ujumbe kwa kipindi cha miaka minne kuanzia tarehe ya uteuzi isipokuwa pale ambapo nafasi ya ujumbe wake itakuwa wazi kutokana na sababu zilizoanishwa kwenye aya ya 10.

Sifa za uteuzi na uidhinishwaji

6. Mtu atastahili kuteuliwa na kuidhinishwa kama mjumbe wa Bodi ya Shule iwapo-

(a) ana angalau Cheti cha Elimu ya Sekondari;

(b) ana kipato kinachotokana na shughuli halali;

(c) sio Diwani, Mwenyekiti, Afisa Mtendaji wa Kiji au Mtaa ndani ya Mamlaka ya Serikali za

Mitaa; na
(d) sio mthibiti ubora kwenye utumishi.

Taratibu ya uidhinishwaji wa wajumbe

7.-(1) Mkuu wa Shule ataandaa orodha ya majina na sifa za wajumbe wa Bodi walioteuliwa katika namna iliyoainishwa na kuwasilisha kwa Mkurugenzi ambako shule ipo kwa ajili ya kuidhinishwa

(2) Mkurugenzi, baada ya kupokea majina ya wajumbe walioteuliwa na sifa zao, atakuwa na mamlaka ya-
(a) kukataa uteuzi wa mjumbe ambaye hajakidhi vigezo vilivyoainishwa chini ya Amri hii na kuagiza uteuzi mwingine; au
(b) kuidhinisha majina ya wajumbe na kumtaarifu kwa maandishi Mkuu wa Shule na nakala kutumwa kwa Mkuu wa Mkoa.

Utolewaji wa barua ya uteuzi

8. Mkuu wa Shule, baada ya kupokea barua ya kuidhinisha majina wajumbe kutoka kwa Mkurugenzi, atatoa barua ya uteuzi kwa wajumbe walioidhinishwa.

Mwenyekiti wa Bodi

9.-(1) Bodi, katika kikao chake cha kwanza, itachagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wajumbe wa Bodi.

(2) Katika Mkutano wa Bodi, iwapo Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataongoza vikao vya Bodi, na endapo wote wawili hawapo, wajumbe waliopo wanaweza kuchagua kutoka miongoni mwao mwenyekiti kwa madhumuni ya kikao husika.

(3) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti waliochaguliwa hawatakiwi kuwa walimu wanaofundisha katika shule husika au mmiliki wa shule hiyo au mwakilishi wake.

Kusitisha ujumbe

10.-(1) Ujumbe katika Bodi ya Shule utasitishwa-
(a) endapo uteuzi utatenguliwa na Mkurugenzi;
(b) endapo mjumbe atajiuzulu kwa hiari kwa kutoa angalau notisi ya maandishi ya siku kumi na nne inayoelekezwa kwa Mkurugenzi wa eneo ambako shule ipo na nakala kuwasilishwa kwa

Mkuu wa Shule;

(c) endapo mjumbe atapoteza sifa zilizomuwezesha kuteuliwa hivyo;

(d) iwapo mjumbe ataondolewa na mamlaka ya uteuzi na kuondolewa huko kutaidhinishwa na Mkurugenzi; na

(e) endapo mjumbe amekufa au kupata tatizo la kudumu kiasi cha kuondoa uwezo wake wa kutekeleza majukumu kama mjumbe;

(2) Pale ambapo mjumbe kipindi chake cha ujumbe kimefikia mwisho kutokana na ukomo wa muda, mjumbe huyo anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.

(3) Iwapo nafasi ya ujumbe wa Bodi itakuwa wazi Mkuu wa Shule ataratibu mchakato wa uteuzi wa mjumbe wa kuchukua nafasi iliyowazi kulingana na masharti na vigezo vya Amri hii

(4) Utaratibu wa kumuidhinisha mjumbe aliyeteuliwa utakuwa kama ulivyoanishwa chini ya aya ya 7 ya Amri hii

(5) Mjumbe aliyeteuliwa atakuwa mjumbe na atahudumu nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki cha mtangulizi wake.

Majukumu ya Bodi ya Shule
Sura ya 353

11.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 39 (1) na (2) cha Sheria, kila Bodi itatakiwa kuzingatia maelekezo ya jumla au mahsusi ya Kamishna.

(2) Bodi itakuwa na uwezo wa kufukuza mwanafunzi kutoka katika shule ambayo Bodi inasimamia.

(3) Bodi itatekeleza mamlaka yake kwa mujibu wa kanuni iliyotungwa na Waziri kwa mujibu wa Sheria.

(4) Kwa nyongeza, Bodi ya Shule itakuwa na majukumu ya ushauri na ushiriki kama ifuatavyo:

(a) kusimamia njia nzuri za ufundishaji na ujifunzaji zenye ufanisi katika shule;

(b) kushauri kuhusu mpango wa maendeleo ya shule na mikakati ya utekelezaji;

(c) kuwezesha uundwaji wa jukwaa la walimu na wazazi;

(d) kuitisha vikao vya walimu na wazazi na kutoa taarifa ya masuala yanayohusiana na maendeleo ya shule;
(e) kushauri kuhusu matumizi sahihi ya fedha katika miradi ya maendeleo ya shule ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule;
(f) kusimamia ujenzi na ukarabati wa madarasa na miundombinu mingine ya shule;
(g) kuhakikisha shule ina miundombinu ya kujitosheleza ikijumuisha madarasa, ofisi, vyoo, maji safi, madawati, ardhi kwa ajili ya michezo na shughuli nyingine za shule;
(h) kuhakikisha kwamba eneo la shule limewekewa mipaka ya kutosha ikiwezekana kujumuisha hati miliki;
(i) kuhakikisha usalama na ulinzi wa wanafunzi, majengo ya shule na mali zake;
(j) kuhakikisha matengenezo ya majengo ya shule na samani;
(k) kuidhinisha bajeti ya mwaka ya shule na matumizi ya fedha za shule;
(l) kukusanya fedha na michango kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa shule;
(m) kuhimiza usafi wa mazingira ya shule na usafi binafsi wa wanafunzi;
(n) kusimamia usajili wa wanafunzi na mahudhurio ya wanafunzi shuleni;
(o) kuhakikisha kwamba shule ina huduma ya kwanza na kuhimiza elimu ya afya; na
(p) kuhakikisha kwamba shule inatoa mwongozo na huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi.

(5) Shule kwa kupitia kwa Katibu wa Bodi itakuwa na wajibu wa kuandaa mambo yote ambayo yanaweza kuwasilishwa kwenye Bodi kwa ajili ya majadiliano isipokuwa pale ambapo dondoo au agenda husika imetoka kwa mjumbe mmoja au zaidi wa Bodi yenyewe.

Vikao

12-(1) Bodi kwa kawaida itakutana mara nne kwa mwaka kwa ajili ya kutekeleza kazi zake katika muda na sehemu itakayoamuliwa kulingana na Kalenda ya Shule iliyoidhinishwa na Bodi kutokana na mapendekezo ya

shule yenyewe.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano maalumu-

(a) baada ya kupokea ombi kwa maandishi kwa niaba hiyo ya wajumbe wasiopungua sita wa Bodi wakieleza kwa undani lengo la kikao hicho na nakala ya notisi pamoja na dondoo au agenda itawasilishwa kwa Katibu angalau siku tano kabla ya kikao hicho maalumu; au

(b) baada ya kupokea notisi ya maandishi kutoka kwa Katibu wa Bodi kuhusu jambo lolote linalohitaji kuwasilishwa kwa haraka na kutolewa maamuzi na Bodi.

(3) Katibu wa Bodi, baada ya kushauriana na Mwenyekiti, ataitisha vikao vya Bodi isipokuwa, vile ambavyo vinaitishwa na Mwenyekiti kwa mujibu wa Amri hii, kwa notisi ambayo itabainisha ajenda, mahali, tarehe na muda wa kikao, na notisi hiyo itatumwa kwa kila mjumbe katika anuani yake ya kawaida kwa njia yoyote ikijumuisha njia ya kielectroniki angalau siku saba kabla ya tarehe ya kikao.

(4) Akidi ya kikao cha Bodi itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe.

(5) Isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo, maamuzi ya wajumbe wengi wa Bodi yatakuwa maamuzi ya Bodi.

(6) Shule itagharamia gharama za uendeshaji wa vikao vyote vya Bodi na gharama hizo zitakuwa ni sehemu ya bajeti itakayoidhinishwa na Bodi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye shule yenyewe.

(7) Katibu ataweka na kutunza taarifa na mihtasari ya mienendo ya Bodi na kuisambaza kwa wajumbe, Mkurugenzi na Katibu Tawala Mkoa.

(8) Kwa kuzingatia masharti ya Amri hii, Bodi inaweza kuweka utaratibu wa uendeshaji wa vikao vyake yenyewe.

(9) Isipokuwa pale ambapo ametangaza kuwa na maslahi, mjumbe wa Bodi hatashiriki katika majadiliano katika kikao au kufanya maamuzi kuhusu masuala yaliyowasilishwa mbele ya Bodi ambayo mwenza wake, ndugu wa damu, mbia au mwajiri, tofauti na serikali, au

mbia au mwajiri wa mwenza wake au ndugu wa damu au vinginevyo, ana maslahi ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja.

Kamati

13. Bodi, katika kutekeleza majukumu yake, itaanzisha Kamati zifuatazo-
(a) Kamati ya Taaluma, Unasihi, Ushauri na Ulinzi wa wanafunzi;
(b) Kamati ya Fedha, Mipango na Maendeleo ya Miundombinu;
(c) Kamati ya Nidhamu, Ulinzi, Mazingira, Afya na Chakula; na
(d) Kamati yoyote itakayoonekana ni ya muhimu kutokana na mapendekezo ya shule.

Mamlaka ya Mkuu wa Mkoa kusimamisha au kuvunja Bodi

14.- Mkuu wa Mkoa anaweza, baada ya kujiridhisha kuwa Bodi imeshindwa kutekeleza kazi na majukumu yake -
(a) kusimamisha Bodi kutekeleza jukumu lake lolote au yote; au
(b) kuagiza kujiuzuru kwa wajumbe wote au mjumbe yeyote na kuagiza kuteuliwa mbadala wake au wao ili kujaza nafasi iliyobaki wazi kwa mujibu wa masharti ya Amri hii.

Kufutwa kwa TS. Na. 417 la 2023

15. Amri ya Uanzishwaji wa Bodi za Shule Zisizo za Serikali ya mwaka, 2023 inafutwa.

Dodoma, …………………, 2024

ADOLF F. MKENDA
*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia*